MTIHANI WA TATHMINI-WILAYA YA NANDI MASHARIKI 2009

102/2
KISWAHILI
(UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMU JAMII)
KARATASI YA PILI
JULAI/AGOSTI, 2009
MUDA: SAA: 2 ½

UFAHAMU:
Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali:

Mjadala kuhusu tohara ya wanawake unaelekea kuchosha akili za watu wngi. Hii ni kwa sababu licha ya kuwepo kwa makundi mengi ya kultetea haki za wanawake, utamaduni wa kuwapasha wanawake tohara ungali ukiendelezwa katika sehemu nying za humu nchini.

Sheria ya Kenya ambayo inapinga wasichana wa umri mdogo kupashwa tohara, sasa inalegezwa na mila za jamii nyingi ambazo zinaendeleza tohara ya wanawake bila kujali hali za mabinti zao. Jamii ambazo zimekataa kabisa kupevuka na kuepuka madhara yanayoletwa na utamaduni huu uliopitwa na wakati.

Lakini swali ni je; nani wa kulumi wa katika suala hili la kushamir kwa tohara ya wasichana? Ni wanume ambao hawachangii katika vita hive? Ni serikali ambayo haipigi msasa sheria za tohara? Au ni makundi ya kutetea haki za wanawake ambayo yamelegea katika kazi zao za kupiga marufuku mila duni kama hizi/ Na je elimu ya kawaida kweli inasaidia katika kuondoa mila hizi za kale/
Majuzi vyombo vya habari viliripoti kisa cha msichana aliyefariki baada ya kupashwa tohara katika eneo la Wajir, Kaskazini mwa Kenya.

Na hata baada ya kisa hiki cha kusikitisha kuripotiwa, idadi kubwa ya wasichana katika sehemu ya Wajir walikuwa wakijitayarisha kwa msimu mwingine wa kupashwa tohara “ili wapate kutimia utu uzima na kuwa wanawake kamili”

MADAI

Hata hivyo, jambo la kushangaza zaidi ni mawazo ya baadhi ya viongozi wa kitamaduni katika eneo la Wajiri.

Ni ajabu kwamba hata baada ya kifo cha msichana huyo(ambaye hakutajwa jina kwa sababu za kisheria) viongozi hao wa kitamaduni wanasistiza kwamba mamake marehemu pamoja na mwanamke aliyehusika na upashaji tohara hawakuwa na hatia kwa kuwa “Kufariki kwa msichana ni ajali to na tunweza kutatua shida hiyo katika baraza la wazee kulingana na utamaduni.”

Wazo kama hili linabainisha wazi kwamba utamaduni mbaya umekuwa donda ndugu miongoni mwa jamii nyingi za humu nchini.

Watu wengi haswa wanaume wanaipuuza tohara kwa madai kwamba suala hili linawahusu wanawake pekee.

Dhana kama hii imechangia katika kuendelea kwa utamaduni huu licha ya mafunzo yanyotolewa kila mara na mashirika ya kutetea haki za wanake.

Dhana kama hii imechangia katika kuendelea kwa utamaduni huu licha ya mafunzo yanayotolewa kila mara na mashirika ya kutetea haki za wanawake.

Lakini pamoja na kwamba idadi kubwa ya wanwake wajikakamua ili kuwaokoa mamia ya wasichana wanaopotoshwa na mila hizi za kale wanawake.

Lakini pamoja na kwamba idadi kubwa ya wanwake wanajikakamua ili kuwaokoa mamia ya wasichana wanaopotoshwa na mila hizi za kale imebainika kwamba baadhi yao wanachochea zaidi katika kutekelezwa kwa utamaduni huo wa kutahiri wasichana.

Bi. Alasa Hussein , mwenye umri wa miaka 39, ambaye alihojiwa na vyombo vya habari baada ya kifo cha msichana huyo kutangazwa, alishikilia kwamba tohara ni njia ya pekee ya wasichana wetu kupitia ili wapate kukubalika katika jamii, bila tohara wsichana wetu hwatakuwa wanawake kamili,"alisema Bi. Hussein ambay mwenyewe ni msomi.

Ikiwa wale ambao wmeelimika wanchangia kushamiri na kukita mizizi kwa desturi hizi za kale, itakuwaje kwa wale ambao hawakuona langa la drasa? Si jamii ina matumaini kwa wale waliobahatika kusoma?

Na si watu waliosoma wanapaswa kulete mabadiliko katika jamii? Kwa mfano, kuhamsisha jamii kuhusu madhara ya kupuuza mambo ya kale kama tohara kwa wanawake?

Kuna uwezakano mkubwa kwamba elimu hapa nchini imekosa maana. Mtu aliyekwenda shuleni akiiga vitendo vya yule ambaye hakusoma ni hatari kubwa katika jamii. Inafaa elimu iwe kama kizazi kipya kwa jamii lakini si kurudisha myuma maendeleo ambayo tayari yalikuwa yakionekena.

Hivyo Bi. Hussein na wengine wenye dhana kama yake wanapaswa kujua kwamba tohara ya wanawake ni suala la mantiki. Na elimu wanayo inatosha kutoa maana ya mantiki hii.

Makundi ya kutetea haki za wanawake pia zinalalamika kwamba vita dhidi ya tohara ya kike "vimekuwa vigumu mno' kwa sababu ya jamii nyingi zenye imani kwamba mila hii ni sehemu ya maisha ya wanawake.

Na ijapokuwa madai hayo ni ya kweli ni bora tujue kwamba pasipo machango wa watu waliosoma, suala la tohara ya wanawake litaendelea kuwepo hata katika karne kadhaa zijazo.

(a) Eleza jinsi mila za jamii nyingi invyolegeza sheria dhidi ya upashaji tohara wa wanawake. (alama 2)

(b) Kulingana na ufahamu ni nani wa kulaumiwa katika suala la ukeketuaji wa wake(na kwa nini) (alama 2)

(c) Jamii inaweza kushughulikia jambo hili kwa njia gain? (alama 4)

(d) Fafanua madhara ya upashaji tohara kwa wake. (alama 4)

(e) Eeza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

(i) Kushamiri:
(ii) Msasa:
(iii) Donda ndugu: (alama 3)

2. UFUPISHO:

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali:

Maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia yamezifikia jamii nyingi za Afrika na maneno mengine yanayondelea kupitia kwa lugha za kigeni, kama vile, Kiingereza na Kifansa, na kupitia

ushirikiano wa sehemu hizi na jamii za kimagharibi. Kutokana na hali hiyo, lugha zilizotumika na zinazoendelea kutumika katika mawasiliano ya kisayansi na kiteknolojia ni hizo za kimagharibi. Wakati huo huo, tunalo jukumu la kuwashirikisha wananchi wengi, ambao hawazijui lugha hizo katika harakati hizi za kimaendeleo ya kisayansi ya pekee na kiteknolojia. Matumaini tuliyonayo ya kutuwezesha kufikia lengo hilo ni ya kuendeleza lugha zetu ambazo zaeleweka na wengi.

Kwa bahati nzuri, teknolojia mpya zinazoibuka pamoja na zile ambazo sasa zimekuwa zikitumika kwa muda hazikuniwa lugha maalum. Lugha yoyote iwayo yaweza kutumiks katika vyombo hivyo. Jambo hilo linasistizwa na Mazrui(1995). Hata hivyo, matumizi ya Kiswahili katika mitambo ya kisasa ya mawasiliano ni finyu mono. Panahitajika harkati madhubuti na mahususi za kuiwezesha itumike zaidi katika vyombo hivi na hili litawezekana tu kupitia kwa juhudi za utafiti.

Manufaa ya mtambo wa kompyuta katika maisha ya sasa ni mengi mno. Hivi sasa kompyuta zinatumika katika sehemu mbali mbali za ulimwengu katika mpango wa elimu ya masafa. Mfumo wa mawasiliano ya mtandao, ambao kimsingi unjuisha uunganishaji wa kmpyuta nyingi duniani, umerahisisha sana ubadilishanaji wa habari. Utafiti wa Kiswahili unaweza kufaidika sana kupitia kwa mfumo huo kwa njia mbili kuu. Kwanza kutokana na hifadhi kuu ya habari katika mfumo huo, mtafiti ataweza kupata habari mbali mbali kutoka kwa vianzo tofauti ambazo zitasaidia kufanikisha utfiti wake.
Pili, itawezekana kufahamu ni maneno gain ambayo yameshafaniwa utfiti hapo awali na watafiti wengine. Kwa vile hatujaunganishwa vilivyo katika mfumo huo, mtafiti mbali zilizofanywa kuhusu lugha ya Kiswahili. Hayo ni baadhi to ya manufaa yanyopatikana kutokana na maendeleo ya teknolojia ya habari ambayo kwa wasiojua lugha za kilimwengu kama kiingereza hwawayapati.

Katika karne hii ya Ishirni na Moja, vifaa vya mawasiliano vimaendelea kuwa changamano zaidi, humku mifumo ya uwashilisaji wa habari ya kisasa ya elektroniki ikiongezeka maradufu. Maendeleo haya ya mawasiliano yanapaswa kuendeleza utu na kuwaleta watu pamoja na wala si kuukengeusha umma.
Hata hivyo, kuna tatizo la lugha.

Kwa kiasi kikubwa maendeleo haya yanafanyika katika lugha ya kiingereza pamoja na lugha nyingine za kilimwengu. Matokeo ni kuwa, kinyume na matarjio, wengi wanishilia kukengeuka; maana wanasikia tu uvumbuzi baada ya mwingine bila kujua hasa kilichovumbuliwa na manufaa yako kwao. Hali hii inadai utafiti wa kuziweka lugha zetu katika hali ya kufaidi maendeleo hayo. Maendeo ya kisayansi na kiteknolojia si milki ya wachance ambao wanelewa Kiingereza, Kijerumani, au Kifaransa na kadhalika kwa upande wetu, pa kuanzia sip engine bali ni kwa Kiswahili.

Ni wajibu wetu basi kuifanyia lugha hii utafiti wa kuiwezesha kutumika katika kufanikisha mawasiliano kwa kupitia mitambo mipya ya kiteknolojia. Twapaswa kuangaza utafiti wetu katika nyanja mbalimbali za kisayansi na kiufundi ili ukosefu wa istilhi usiendelee kutolewa kama mokawapo ya sababu zizuiazo matumizi ya Kiswahili katika ngazi mbalimbali. Kuna umuhimu wa kuongeza kasi ya mrdi wa utafiti utakaozalisha msamiati wa kompyut; hali ambayo itapelekea kuwa na Kiswahili katika kompyuta ambayo ni kiini cha vyombo vingine vya mawasiliano ya kisasa.

(makala ya Mohochi H. Katika, utafiti wa Kiswahili uk. 221-222)

Maswali:

(a) Kuimarishwa kwa hadhi ya Kiswahili kuna manufaa gain kulingana na makal haya? (maneno 60-70) (alama 4, 1-Mtiririko)

Matayarisho

Jibu

(b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 90-100) (allama 8,2-Mtiririko)

Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA:

(a) Toa mifano miwili kwa aina zifuatazo za sauti.
  (i) Nusu-irabu (alama 1)
  (ii) Vimadende: (alama 1)

(b) tunga sentensi tatu kubainisha maana tofauti za neon kitovu (alama 3)

(c) Ainisha neon lifuatalo:
  Alinijia (alama 2)

(d) Tunga sentensi kuonyesha:
  (i) Kirai kivumishi; (alama 1)
  (ii) Kirai kihusishi (alama 1)

(e) Changanua sentensi ifuatayo kea kutumia mstari:
  Mpishi aliyeleta chakula ameondoka hivi sasa. (alama 3)

(f) Nyambua vitenzi vifauatavyo katika kauli zilizo kweny mabano:
  (i) pwa (Kutendwa) (alama 1)
  (ii) Ja (kutendesha) (alama 1)

(g) Onyesha shamirisho kitondo, kipozi na al katika sentensi ifuatayo:
Kipkemboi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari. (alama 3)

(h) Yakinisha:
  (i) Msipowachokoza wenzenu hamtaadhibiwa (alama 3)

(i) Tunga nomino ifuatayo sentensi kuonyesha upatanisho wa kisanfi ukitumia 'a' unganisfu;

  Upasuaji (alama 1)

(j) Tambua aina mbili za vielezi na mbili za viumishi vinavyopatikana katika sentensi:
Wale wanariadha wawili walikimbia jana kwa bidii na kubuka na ushindi. (alama 4)

(k) <u>Eleza maana mbili za sentensi:</u>
Jua nisemalo ni muhimu kwetu. (alama 2)

(I) <u>Tumia vielezi vifuatayo kama nomino katika sentensi</u>:
  (i) Haraka: (alama 1)
  (ii) Kimya: (alama 1)

(m)<u>Tambulisha aina za vitenzi vilivyotumia katika sentensi ifuatyo:</u>
  Nina kurina asali leo. (alama 2)

(n)<u>Tunga sentensi tatu kubainisha matumizi tofauti ya neon- KWA:-</u>

(o) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia ngali:
(alama 1)

Alichora akatuzwa. (alama 1)

(p) Tunga sentensi moja kwa kutumia kiwakilishi cha idadi.
(alama 1)

(q) Andika kinyume cha:

Kijana aliyekwea mlima alisifiwa na mwalimu. (alama 1)

(r) Akifisha kifungu kifuatacho:

Unasemaje sema na ni nisikie mi sipendi kusema na mtu aknipa mgongo kama nnasema ha kuvuli. (alama 4)

ISIMU JAMII

(a) (i) Nini maana ya lafudhi? (alama 2)

(ii) Taja mambo mawili yanayosababisha kuibuika kwa lafudhi (alama 2)

(b) Fafanua kaida tatu ambazo lugha lazima izingatie ndipo iweze kutumika kama lugha ya taifa.